# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA WAZIRI MKUU,

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.

## SHULE YA SEKONDARI PAMOJANGABOBO

**MKOA:** ARUSHA
**HALMASHAURI:** MERU
**KATA:** NGABOBO

**SANDUKU LA POSTA:** 102 USA – RIVER
**BARUA PEPE:** pamojangabobo2019@gmail.com

**Kumb Na: PNSS/J.1/VOL.3/2025**

**+255 748 298 572 NAMBA YA SIMU YA SHULE**
**+255 757 270 772 MKUU WA SHULE**
**+255 768 510 175/ +255 745 309 242 MAKAMU MKUU WA SHULE**
**+255 753 152 435/ +255 682 882 745 PATRON/MATRON**

**PICHA YA MWANAFUNZI**

Mzazi/mlezi wa mwanafunzi …………………………………………………………………

S.L.P …………………………………………………………………………………………………

**Yah: <u>KUCHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI PAMOJANGABOBO HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU MKOA WA ARUSHA MWAKA</u>** ……………..

Ninayo furaha kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha TANO Tahasusi (combination) PCM ☐ PCB ☐ na HKL ☐ (***Weka alama √ kwenye kisanduku katika combination uliyochaguliwa)*** katika shule hii mwaka ............. Ninatumia fursa hii kukupongeza wewe na mwanao kwa hatua hii muhimu ambayo mwanao anaiendea hongereni sana.

Shule itafunguliwa Tarehe ……………….. mwanafunzi atatakiwa kuripoti shuleni Tarehe …………………. na mwisho wa kuripoti ni Tarehe………………….

### MAHALI SHULE ILIPO

Shule hii ipo katika kata ya Ngabobo, Halmashauri ya Meru, Wilaya ya Arumeru, Mkoa wa Arusha umbali wa kilomita 36 kutoka Makao Makuu ya Wilaya yetu ya Arumeru. Pia kwa upande wa Ngabobo madukani sehemu ambayo ni mwisho wa gari shule ipo umbali wa kilometa 2.

Shule hii ilianzishwa mwaka 2019 na ina kidato cha Kwanza (I) hadi cha Sita (VI). Shule ni ya bweni kwa kidato cha Kwanza (I) hadi cha Sita (VI). Pia shule yetu ni ya mchanganyiko wa jinsia ya kiume na kike.

### NAMNA YA KUFIKA SHULENI

Kwa usafiri wa moja kwa moja mwanao atapanda basi la **URIO SAFARIS** kutoka stendi kuu ya Mabasi Arusha au Usa-River, basi ambalo limeandikwa Ngabobo Pamoja. Basi hilo hufika hapa shuleni mara moja moja, hivyo ikitokea limeishia Ngabobo madukani, mwanao atapanda pikipiki kwa nauli ya shilingi 3,000/= Nauli ya basi kutoka Arusha mjini hadi Ngabobo ni shilingi 6,000/= kwa sasa lakini Basi hilo kila siku hufika Ngabobo madukani muda wa jioni saa moja mpaka saa mbili.

Usafiri mwingine wa kufika shuleni ni kwa kutumia magari aina ya **Noah** ambayo huanza safari zake Usa – River mpaka Ngarenanyuki (Olkung'wado) kwa nauli ya Tsh 6000/=, mwanao atapanda pikipiki mpaka shuleni kwa

maelewano ya nauli kuanzia Tsh 8000/= hadi Tsh 12,000/=. Usafiri huu wa kutumia Noah husaidia kufika shuleni mapema mchana.

## MAHITAJI MUHIMU YA KUZINGATIA

### 1. FEDHA

i. Tahadhari (caution money) Tsh. 5,000/= fedha hii haitarejeshwa
ii. Gharama ya uendeshaji Tsh 65,000/=
iii. Kitambulisho Tsh 5,000/=
iv. Nembo Tsh 5,000/=

JUMLA Tsh **80,000/=**

Fedha zote zilipwe kwenye akaunti ya shule namba **43210009336** yenye jina la **Pamoja secondary school Recurrent Account benki ya NMB**. Wakati wa kulipa andika jina kamili la mwanafunzi na. kwenye pay in slip, hii ni muhimu sana kwa ajili ya kumbukumbu za kiofisi. Iwapo mwanao anafadhiliwa na serikali kuu, Halmshauri au Shirika/Taasisi yoyote, huna budi kuwasilisha uthibitisho rasmi kabla ya kupokelewa/ kusajiliwa shuleni.

### 2. SARE YA SHULE (SCHOOL UNIFORM)

**Kwa wavulana**

i. Mashati mawili (2) meupe ya mikono mirefu.
ii. Suruali mbili (2) za kitambaa rangi nyekundu yenye mkanda mweupe pande mbili katika kila mguu. Upana wa suruali kwa chini ni sentimita 16 na iwe na marinda mawili kwa kila upande. Hairuhusiwi kubana suruali kuwa mnyonyo (modo) au kuvaa mlegezo hapa shuleni.



***(Sample ya suruali nyekundu yenye mkanda mweupe)***

iii. Sweta mbili (2) za rangi nyekundu yenye mistari meupe kwenye shingo na mikono.
iv. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga kwa kamba na vinavyopigwa rangi na visiwe na visigino virefu (highhills) jozi mbili (2). Buti za jeshi haziruhusiwi hapa shuleni.
v. Soksi nyeusi jozi tatu (3).
vi. Tracksuit (1) ya rangi ya bluu bahari yenye mistari meupe kwa kila mmoja.
vii. Tai mbili (2) za rangi nyekundu isiyo na mistari meupe.
viii. T-shirt 2 zenye shingo ya collar (form Six) na rangi za kijivu (gray) (Kwa ajili ya shamba drees)
ix. Suruali 2 za rangi ya dark blue upana wa sentimita 17 miguuni (isiyobanwa) (Kwa ajili ya shamba dress)



***(sample ya suruali dark blue)***

**Kwa wasichana.**

i. Mashati mawili (2) meupe mikono mirefu.
ii. Sketi (2) za drafti rangi nyekundu ndefu hadi kifundo cha mguu. **Angalizo:** Sketi fupi zinazoishia kwenye magoti au juu ya magoti hazitaruhusiwa hapa shuleni kabisa.



***(sample ya sketi draft rangi nyekundu)***

iii. Sweta mbili (2) za rangi nyekundu yenye mistari meupe kwenye shingo na mikono.
iv. Viatu vyeusi (juma na rosa) jozi mbili.
v. Soksi nyeupe (stocking) jozi nne (4).
vi. Tracksuit ya rangi ya bluu bahari jozi moja.
vii. Tai mbili (2) za rangi nyekundu isiyo na mistari meupe.
viii. T-shirt 2 zenye shingo ya collar (form Six) na rangi za kijivu (gray) (Kwa ajili ya shamba drees)
ix. Sketi 2 za rangi ya dark blue ndefu mpaka kwenye kifundo cha mguu (Kwa ajili ya shamba dress)



***(Sample ya sketi rangi dark blue)***

***Sample ya sweta la shule (kwa jinsia zote)***



***Sample ya T-shirt ya shule (kwa jinsia zote)***



***Sample ya Tai (kwa jinsia zote)***



### 3. VIFAA VYA MICHEZO

i. Bukta ya rangi nyeusi 2.
ii. T- Shirt ya rangi nyeusi moja.
iii. Raba za michezo jozi moja.
iv. Soksi nyeusi jozi mbili.

### 4. MAHITAJI YA MALAZI BWENINI.

i. Godoro moja la sponji lenye upana wa futi mbili na nusu 2.5m.
ii. Shuka mbili za rangi ya **bluu bahari** kwa wavulana na rangi ya **pinki** kwa wasichana.
iii. Blanketi moja.
iv. Nguo za kulalia (night dress).
v. Sanduku imara la kuhifadhia mali zako. Tafadhali liwe moja la chuma lenye kofuli.
vi. Mahitaji ya usafi binafsi mfano: sabuni ya kufulia ya mche, sabuni ya unga, mafuta ya kujipaka, mswaki na dawa ya meno.
vii. Ndoo mbili ndogo kwa ajili ya usafi (kuogea na kufulia) na kuhifadhia maji.
viii. Chandarua 1
ix. Taulo za kike *(Pedi)* kwa wasichana tu. Pakiti tano (5)


**NB:** Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo ya aina nyingine tofauti na zilizotajwa katika fomu hii.

### 5. VIFAA KWA AJILI YA CHAKULA.

Mwanao atapaswa kuwa na sahani ya aluminium moja, kijiko kimoja na kikombe kimoja cha aluminium. Vyote hivi vinapatikana kwenye duka la shule.

### 6. MAHITAJI YA TAALUMA.

i. Begi zuri la kubebea madaftari na vifaa vya masomo.
ii. Madaftari makubwa (counter books 4Q) yasiyopungua 8 kwa ajili ya masomo.
iii. Rimu za makaratasi (04); mbili (2) ya mistari (ruled) na mbili (2) ya A4 aina ya **TRION**, **DOUBLE A**, **ARTWORK premium multipurpose business paper**, **PAPERLINE** na **aOne** kwa ajili ya mitihani ya ndani. **ANGALIZO:** Zingatia kuja na aina ya karatasi (rimu) nyeupe (plain papers) kwenye orodha iliyotajwa hapo juu.










iv. Mathematical instruments (vifaa vya Hisabati) kwa wale wa PCM na PCB tu.
v. Scientific calculator fx 991 kwa wale wa PCM na PCB tu.
*vi.* Koti moja rangi nyeupe *(mwanafunzi huvaa wakati wa ujifunzaji kwa vitendo maabara kwa masomo ya sayansi yaani wakati wa practicals).* Kwa wanafunzi wa PCM na PCB tu.
vii. Miwani mikubwa ya macho *(Eye goggles kwa matumizi ya maabara)* PCM na PCB tu.
viii. Gloves boksi moja dogo. *(kwa matumizi ya maabara)* PCM na PCB tu.
ix. Viziba pua na mdomo pakti moja *(Mouth and nose mask kwa matumizi ya maabara)* PCM na PCB tu.
x. Buti nyeupe jozi moja *(Huvaliwa wakati wa ujifunzaji kwa vitendo maabara)* PCM na PCB tu.
xi. Dissecting kit. *(PCB pekee)*

**Vitabu vya ziada: kila mwanafunzi anapaswa kuwa na vitabu vya ziada kama ilivyo kwenye orodha hapo chini kulingana na masomo: -**

**PURE MATHEMATICS**

- Pure mathematics I and II by J.K.Backhouse
- Advanced level PURE mathematics by Kinunda
- Advanced level PURE mathematics by C.J.Tranter – 2006
- S. Chand mathematics for class XI, VOLUME I and II by H.K. DASS R. VERMA 2013

**CHEMISTRY**

- Conceptual chemistry for class XI by S. Chand (brown cover – not written volume)
- Conceptual chemistry for class XII by S. Chand (blue cover – Not written volume)
- Chemistry for advanced secondary school's student's book form five. By T.I.E
- Chemistry for advanced secondary school's student's book form six. By T.I.E

**PHYSICS**

- Principles of Physics class XII By S. Chands.
- Principles of Physics class XI By S. Chands
- Advanced level Physics by Nelcon & Parker
- Physics for advanced secondary school's student's book form five. By T.I.E
- Physics for advanced secondary school's student's book form Six. By T.I.E
- Physics student's book. By Rojaman Casta

**HISTORY**

- The political economy, emperialism by Nabudere
- Mastering advanced level History book II by Kato
- Major events in the world History Paper II Advanced level by Gervas m, Zombwe.
- World advanced level by Samwel Mhajida

**KISWAHILI**

***I. USHAIRI:***

- Kimbunga – G.Gora (Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili )1999
- Mapenzi bora – S. Robert (mkuki na nyota)
- Fungate ya uhuru – M.S. Khatibu

***II. RIWAYA:***

- Vuta n' Kuvute - A.Shafi (mkuki na nyota)
- Mfadhili – Hussein Tuwa
- Usiku unapokwisha – Mbunda Msokile

***III. TAMTHILIA:***

- Moran E. Mbogo
- Kivuli kinaishi – Said Mohamed 2007
- Kwenye ukingo wa Thim – E.Hussein
- Nguzo mama 1982

**ENGLISH LANGUAGE**

- Advanced level English language 1 form 5&6 by Ndambo S. and Kinunda J.
- English for advanced level sec schools form 5 by T.I.E
- English for Advanced sec schools form 6 by T.I.E

- English language for Advanced level by Shaban Shafii

Advanced level English Competence Based Approach by Nicholaus Asheli.

*i.* ***NOVEL***

- The beautifull Ones are not yet Born by A.K.Amah
- A man of the people By C.Achebe.
- His Excellence the Head of State.
- Divine providence by Mkuki na Nyota
- Encounters from Africa by Macmillian.

*ii.* ***PLAYS / DRAMA***

- An enemy of the people H.Ibsen
- I will marry when I want – EAEP
- Lwanda Magere by Okot Omtatah – 1991
- Betray in the city by Francis Imbunga

*iii.* ***POETRY***

- Selected Poems from Institute of Education
- The wonderful surgeon and other poems – Mkuki na Nyota

**BIOLOGY**

- Biological science (BS)
- Biology for Advanced Level Secondary School form 5 by T.I.E

**GENERAL STUDIES**

- Understanding General studies for A Level by Johanes Big Wamungu 2015

**COMPUTER SCIENCE**

- Computer sciences for advanced secondary school's student's book form five. By T.I.E
- Computer sciences for advanced secondary school's student's book form six. By T.I.E

## 7. VIFAA VYA USAFI WA MAZINGIRA, BWENI NA MADARASA.

**Wavulana.**

***a)*** Squeezer (mopa) moja
***b)*** Fyekeo moja.
***c)*** Jembe moja na mpini wake.

**Wasichana.**

**a)** Soft broom moja
**b)** Fyekeo moja
**c)** Jembe moja na mpini wake

**NB:** Malipo yote yalipwe katika akaunti ya shule tajwa hapo juu.Mwanafunzi atasajiliwa endapo atakuwa amezingatia na kutimiza maelekezo yote yaliyoainishwa kwenye fomu hii. Zingatia kuepuka usumbufu. Mwanafunzi atatakiwa kurudisha fomu hii ikiwa imejazwa kikamilifu.

……………………….

**JOHN P. AWE**

**MKUU WA SHULE**

**OFISI YA WAZIRI MKUU,**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.**
**SHULE YA SEKONDARI PAMOJANGABOBO**

**FOMU YA TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI.**

**SEHEMU A. *i/* IJAZWE NA MWANAFUNZI**

1. Jina kamili……………………………………………………………………………………..
2. Tarehe na Mwaka wa kuzaliwa…………………………. Dini……………………………….
3. Mahali alipozaliwa kijiji/mtaa………………………………… kata…………………………..
   Tarafa…………………………… wilaya………………………….. Mkoa ………………………….
4. Shule alipomalizia kidato cha nne(4)…………………………………………………..
5. Umewahi kuwa kiongozi shuleni *(Jibu Ndiyo au Hapana)* ……………………..
6. Michezo unayopendelea…………………………………………………………..

***ii/.* TAMKO LA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI PAMOJANGABOBO.**

Mimi……………………………………………………………… Nimezisoma na kuzielewa sheria, kanuni na taratibu za shule na kwamba niko tayari / siko tayari kuzifuata na kwamba sitajihusisha na uchochezi au mgomo wowote katika maisha yangu yote ya shule.

Sahihi ya mwanafunzi………………………..

**PICHA YA MZAZI/MLEZI.**

**SEHEMU B. IJAZWE NA MZAZI/ MLEZI WA MWANAFUNZI.**

1. Jina la mzazi/ mlezi……………………………………………… simu ………………………..
2. Kazi na nawani ya mzazi/mlezi ……………………………………………………………..
3. Namba ya kitambulisho cha Taifa (NIDA)……………………………………………………….
4. Mtoto anaishi na ……………………………………………………………………………
5. Dini ya Baba ………………………….. Dhehebu ……………………………………..
6. Dini ya mama …………………………..Dhehebu ……………………………………….
7. Dini ya mtoto …………………………...Dhehebu ……………………………………….
8. Anwani kamili ya nyumba ambako mtoto atakuwa anakwenda siku za likizo
   ……………………………………………………………………………………………………

**TAMKO/AHADI YA MZAZI/MLEZI.**

Mimi ……………………………………………………………………………… Baba/mama/mlezi wa ……………………………………………………………… Nathibitisha kuwa taarifa hiyo hapo juu ni sahihi na ninaahidi kushirikiana na uongozi wa shule kujenga nidhamu, taaluma, juhudi na maarifa kwa mwanangu katika kuitikia wito wake kielimu na kwamba nitatekeleza maagizo na mahitaji yote ya shule kama nilivyoelekezwa.

Tarehe …………………………………………. Sahihi ya Mzazi/Mlezi ……………………………………….

**SEHEMU C: IJAZWE NA AFISA MTENDAJI WA KIJIJI /MTAA**

Mimi ……………………………………………………………………… ninathibitisha kuwa ndugu …………………………………………….. ni mzazi/ mlezi wa Mwanafunzi……………………………………na taarifa za mtoto na mzazi/mlezi ni sahihi. Ninaahidi kutoa ushirikiano wa kila namna pindi tatizo litakapotokea muda wote kijana awapo shuleni.

Saini na Mhuri wa afisa mtendaji………..………….. Namba ya simu………………… Tarehe………………….

**<u>KABLA YA KUJA SHULENI VEMA KUTIMIZA YAFUATAYO: -</u>**

i. Aje na nakala ya cheti cha matokeo ya kidato cha nne (*result slip*) na cheti cha kuzaliwa (nakala).
ii. Kupimwa na daktari wa hospitali inayotambulika serikalini. Tumia Fomu iliyoambatanishwa.
iii. Kusoma na kuzielewa sheria/ kanuni za shule (zimeambatanishwa)
iv. Kujaza fomu ya maelezo yanayohusika pamoja kubandika picha ya paspotsize ya mwanafunzi na mzazi/mlezi.
v. Mwanafunzi haruhusiwi kuja na **simu** shuleni kabisa

**SHULE YA SEKONDARI PAMOJANGABOBO**

**SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu No. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria namba 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na ufundi yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi Ya Rais. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

**A. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

1. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
2. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
3. Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (Preparation).
4. Kuwahi katika kila shughuli zilizopo katika ratiba ya shule na nyingine utakazopewa.
5. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
6. Kutunza usafi wa mwili mfano kukata kucha, kunyoa ndevu, na kunyoa nywele (nywele ndefu haziruhusiwi hapa shuleni). Mavazi na mazingira ya shule yawe safi muda wote. (Ni marufuku kutupa taka hovyo mfano karatasi, chupa na maganda ya matunda).
7. Kuvaa sare kamili ya shule wakati wote unapotakiwa (Outfits that are tight, short, or transparent clothes are not allowed. Shorts only allowed for games).
8. Kuwepo kwa wakati sehemu zote mwanafunzi anapohitajika na kuzingatia ratiba ya shule ilivyoelekezwa.
9. Ratiba na vipindi vyote vya ibada ufuatwe na kila mwanafunzi kwa imani yake.

**B. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE.**

1. Wizi wa mali za shule au ya mwanafunzi mwenzako.
2. Uasherati/ Uzinzi/ ulawiti/ ubakaji na ushoga.
3. Ulevi wa aina yoyote (pombe, mirungi na aina zingine zote za madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine kuberi, sigara, n.k)
4. Kupiga au kupigana na mwanafunzi au mwalimu/mtumishi yeyote wa shule.
5. Kuharibu kwa makusudi mali ya shule au ya mwanafunzi mwenzako.
6. Kudharau bendera ya Taifa.
7. Kuoa/kuolewa, kubeba mimba au kusababisha mimba.
8. Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo, kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
9. Kukataa/kumgomea mwalimu adhabu kwa makusudi.
10. Kukutwa nje ya shule pasipo ruhusa maalum kutoka uongozi wa shule.
11. Kukutwa au kumiliki simu ya mkononi au vifaa vyake mf. Line, charger, betri ya simu na vifaa vingine vya umeme kama Mp3 players na chaja yake.
12. Kulala nje ya shule pasipo ruhusa maalum kutoka uongozi wa shule.
13. Kukamatwa kwenye Mahusiano ya kimapenzi kati ya mwanafunzi na mwanafunzi au mwanafunzi na mtumishi wa shule hii au mwanafunzi na mtu mwingine yeyote nje ya shule.
14. Kutishia au kujiua/kujitoa uhai.
15. Kukutwa sehemu zifuatazo:a) Makazi/ nyumba za watumishi wa shule hii.

b) Kwenye kumbi za starehe na burudani.
c) Vilabu vya pombe.
d) Utoro wa siku tisini (90) mfulululizo bila taarifa.
e) Kutoa lugha chafu za matusi kwa wanafunzi, walimu na watumishi wengine.
f) Kufuga ndevu na nywele (wanafunzi wate wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote).

**…………………………..**

**JOHN P. AWE**

**MKUU WA SHULE**

**PRIME MINISTER'SOFFICE.**
**REGIONAL ADMNISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT.**

**PAMOJA NGABOBO SECONDARY SCHOOL**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

To be completed by Medical officer in a Government Hospital in respect of all new entrants to Pamoja Ngabobo secondary school.

Pamoja Ngabobo sec. school
P. O. Box 102,
Usa – River

To the Officer,
………………………………..,
P. O. Box……………..,
…………………………

Full name *(student name)* ……………………………………………………. Age ………
Please examine the above named as to his / her physical and mental fitness for a full-time secondary school studies that may also include military training. The examination will include the following categories of which will render the applicant's ineligible in case of a defect.

1. AIDS test ………………………………………………
2. Blood count (red & white) ………………………………
3. Urine examination ……………………………………………
4. Stool examination ………………………………………………
5. Syphilis test …………………………………………………
6. T.B test …………………………………………………
7. Ear test ……………………………………………………………
8. Eye test ……………………………………………………………
9. Spleen test ……………………………………………………
10. Abdomen test …………………………………………………
11. Additional information or any other physical, mental, hereditary or intoxication diseases.
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
12. Other serious diseases
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

I certify that the above mentioned has been examined and found it to/ not to pursue further education.

Signature ……………………………………………………….

Designation ……………………………………………………

Station …………………………………………………………

Date …………………………………………………………..

Official stamp ……………………………………………….